

# TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII-TENGERU



## MAFUNZO YA ZIADA YATAKAYOLEWA CHUONI TICD KWA KUSHIRIKIANA NA JOBORTUNITY TANZANIA KUANZIA TAREHE 06/APRILI/2019

### 1. UTANGULIZI

Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali (Jobortunity) wameungana kuanzisha program maalumu (extra curriculum) kwa wanachuo wa maendeleo ya jamii ili kuwajengea uwezo wa kimtazamo chanya ili kumudu mazingira ya kimaisha, utendaji kazi mara baada ya kumaliza elimu yao na kuwajengea nguvu ya ushindani kwenye soko la ajira.

### 2. AINA YA MAFUNZO YATAKAYOTOLEWA NA MUDA WA KUANZA MAFUNZO

Aina ya mafunzo yatakayotolewa na program hii ni ya mtindo ujulikanao kama Hi 5, maana yake ni kila kidole katika mwili wa binadamu kina maana yake, na endapo vidole vyote vitatumika ipasavyo, kijana atakua amekamilika kwa maana ya kuwa na mtazamo chanya, kujiamini, kujitambua, kuwa na maadili yatakiwayo sehemu za kazi na maisha kiujumla. Programu hii itanza kutolewa muhula wa pili wa masomo hapo tarehe **06/Aprili/2019**. Kujiunga kwenye programu hii ni hiyari ya mwanafunzi husika akizingatia faida zifuatazo.

### 3. FAIDA KWA ATAKAYEJIUNGA NA PROGRAMU HII;

- Kumwezesha kijana kujitambua na kujiamini mbele ya halaiki yoyote
- Kumjengea uwezo wa kujiandaa na masuala ya ajira kabla na baada ya kuhitimu mafunzo yake.
- Kumuongezea uwezo na kumpa mbinu za kubaliana na changamoto zilizopo kwenye soko la ajira
- Kumjengea uwezo wa kimtazamo juu ya maisha ya ajira na kujitegemea
- Kumjengea uwezo wa namna ya kujiwasilisha mbele ya jamii
- Mwisho wa mafunzo mshiriki atatunukiwa cheti maalum ambacho ni chachu ya kuajiriwa kwa Taasisi na mashirika mbalimbali nchini Tanzania na kwingineko.
- Kuingizwa kwenye mtandao wa utafutaji wa ajira kwa urahisi na uharaka.

#### **4. GHARAMA YA KUJIUNGA NA PROGRAMU HII**

Gharama za kujiunga na programu hii ni **Tshs. 350,000/-**. Kwa kutambua umuhimu wa programu hii kwa wanafunzi wake Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa kushirikiana na Jobortunity (Shirika lisilo la kiserikali kutoka Uholanzi lenye kituo chake cha mafunzo jijini Arusha) wamekubaliana kuwa watagharimia **Tshs. 250,000/-** na kiasi kinachosalia ambacho ni **Tshs. 100,000/-** kitalipwa na mwanafunzi atakayeridhia kujiunga na kushiriki.

***Kwa maana hiyo, mshiriki atapaswa kujiunga kwa Tshs. 100,000/- hadi mwisho wa mafunzo.***

#### **5. MUDA WA PROGRAM NA MAHALI MAFUNZO YATAKPOFANYIKA**

Program hii itaanza mara baada kufungua chuo (tarehe 06/ Aprili/2019), kwa kila siku za Jumamosi na Jumatano kwa muda wa wiki tano (05).

#### **6. TARATIBU ZA MALIPO**

Malipo yote yafanyike kupitia benki kwa akaunti namba:

***Jina la Akaunti: Jobortunity LTD***

***Akaunti namba: 0260000425***

***Bank: Exim Bank***

#### **7. MAWASILIANO:**

*Mr Daniel S.Wambura (Mratibu wa Program - TICD)*

*Simu: 0744146581/0621269665*

*Email: [danel.wambura@tcdti.ac.tz](mailto:danel.wambura@tcdti.ac.tz)*

*Mr Utonga Dickson (Mratibu wa Program-TICD)*

*Simu:0752278199*

*Email:dickiedannie@gmail.com*

*Mis Grace Chwezi(Mratbu wa Programu-Hi 5)*

*Simu:0755883458*

#### **MUHIMU:**

Ilikujiunga na program hii, tafadhali jaza fomu iliyoambatanishwa na kuiwasilishwa kwenye ofisi ya msajili chuoni.